**HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**

**KATA YA UYOGO**

**SHULE YA MSINGI NSUNGA**

**MTIHANI WA KUMALIZA MUHULA WA PILI 2025**

**SOMO LA URAIA NA MAADILI DARASA LA V**

**JINA:**________________________________________________

**MAELEKEZO KWA MTAHINIWA** 1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C yenye jumla ya maswali sita (06)2. Jibu maswali yote katika kila sehemu **SEHEMU A ( ALAMA 20 )**

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

1. **Katika kipengele (i) – (x) , chagua jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu sahihi.**

(i) Mtu anapata uraia wa Tanzaniakwa kuzaliwa, kurithi na :
(a) Kuwatembelea wazazi wanaoishi Tanzania (b) Kutumia kitambulisho cha mpiga kura (c) Kujiandikisha (d) Kwa kuishi miaka mingi Tanzania ( e) Kupewa

(ii) Tofauti ya kimaumbile kati ya mwanaume na mwanamke hujulikana kama_________
(a) Jinsi (b) Jinsia (c) Tofauti ya kijinsia (d) Usawa wa kijinsia ( e) Kimaumbile

(iii) Mkuu wa wilaya anapatikanaje ?
(a) Kupigiwa kura na madiwani (b) Kuajiriwa na menejimenti ya utumishi wa umma (c) Kuteuliwa na Rais (d) Kupigiwa kura (e) Kuchaguliwa na wananchi

(iv) Shughuli za maendeleo ya jamii ni pamoja na :_________________
(a) Kuiba na kutapeli wenzako (b) Kuharibu mazingira (c) Kusafisha barabara, mitaro na mazingira (d) Hakuna jibu sahihi ( e)Kusoma kwa bidii

(v) Ipi kati ya zifuatazo ni faida ya kuchangamana na watu tofauti?
(a) Uendo na kuheshimiana(b) Ubaguzi (c) Kutokuthamini utu (d) Kuleta migogoro (e) kufilisika

(vi) Kuwa na uhuru wa kutoa maoni ni moja ya nguzo za_________(a) Kutii sheria (b) Demokrasia
( c) uwajibikaji (d)udikteta (e)majukumu

(vii) Je, utafanya nini kutatua tatizo lililo nje ya uwezo wako ?
(a) Kulikubali na kuomba ushauri kutoka kwa watu unaowaamini (b) Kuepukana nalo (c) Kulipuuzia (d) Kulifikiria kwa makini (e )kusimulia watu

(viii) Tathmini ya utekelezaji wa malengo hufanyika wakati gani ?
(a) Wakati wa utekelezaji (b) Baada ya utekelezaji (c) Wakati na baada ya utekelezaji (d) Wakati wowote (e ) kabla ya utekelezaji

(ix) Yafuatayo ni madhara ya kutokuwa muwazi
(a) Kusifiwa na kuharibu (b) uzembe na uhalifu (c) mshikamano na uvivu (d) kujenga chuki ( e) kuleta migongano

(x) Jumuiya ya kimataifa iliyokubwa kuliko zote duniani ni
(a) Jumuiya ya madola (b) Umoja wa Afrika (c) Jumuiya ya maendeleo kusini mwa Afrika (d) Umoja wa mataifa ( e) Jumuiya ya Afrika Mashariki

2. **OANUSAHA KUNDI A(A) NA (B),**

| KUNDI A | MAJIBU | KUNDI B |
|---|---|---|
| (i) 12 Januari | | A:Sikukuu ya wafanya biashara |
| (ii) 01 Mei | | B:Sikukuu ya wakulima |
| (iii) 07 Julai | | C:Kumbukumbu ya cha kifo cha karume |
| (iv) 07 April | | D:Sikukuu ya mapinduzi ya Zanzibar |
| (v) 14 Oktoba | | E:Sikukuu ya wafanyakazi |
| | | F:Kumbukumbu ya kifo cha nyerere |

**chagua maneno sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuyaandika katika nafasi uliyopewa**

| **staha, dola, masuuli, hewa ya naitrojeni, nasaha,mazungumzo ,hewa ya ukaa, mkakati** |
|---|

(i) Mawaidha,mashauri au mwongozo mzuri katika jambo________________________________

(ii) Heshima na Adabu________________________________________

(iii) Hewa yenye sumu ya kaboni inayotokana na uchafuzi wa mazingira_____________________

(iv) Kuwajibika kwa masuala yote yanayohusu uendeshaji,usumamizi na uidhinishaji wa fedha_______________________________________________

(v) Chombo chenye mamlaka ya kuendesha utawala au siasa ya nchi_______________________

**SEHEMU B ( ALAMA 20 )Jibu maswali yote katika sehemu hii**

3. Katiba yetu ya mwaka 1977 ina jumla ya sura kumi. Kwa kutumia sentensi zifuatazo zipange kulingana na sura tano za mwanzo zilizopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzipa namba ( 6 - 10 )
   (i) Sura ya ( ) : Inahusu majeshi ya ulinzi na Madaraka ya amiri jeshi mkuu
   (ii) Sura ya ( ) : Inahusu tume ya haki za binadamu na utawala bora na sekretarieti ya maadili ya viongozi wa umma
   (iii) Sura ya ( ) : Inahusu Madaraka ya umma katika serikali za mitaa na kazi za serikali za mitaa
   (iv) Sura ya ( ) : Inahusu menyineyo mfano jina la katiba,tarehe ya kuanza kutumika katiba hiyo
   (v) Sura ya ( ) : Inahusu masharti kuhusumchango wa serikali na mambo yote ya fedha zinazoingia katika hazina ya serikali ya Jamuhuri ya Muungano

**Andika jibu sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.**

(i) ____________________________ni kuhoji au kupeleleza kwa lengo la kujua zaidi.
(ii) Juma na Zauda wana tabia ya kupenda nchi yao.Je ni tabia Juma na Zauda wanaonesha kwa wengine_________________________
(iii) ___________________ni alama ya taifa inayotumika kama muhuri wa nyaraka za serikali
(iv) Kiongozi wa juu zaidi katika ngazi ya Mkoa ni_____________________________
(v) __________________________maarifa ya sayansi yaliyowekwa katika matumizi

**SEHEMU C ( ALAMA 10 )Jibu maswali yote katika sehemu hii.**

4. Soma kwa makini kifungu cha Habari kifuatacho kisha jibu kipengele (i-v) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.
   Hawa ni mwanafunzi wa darasa la tano katika shule ya msingi Huruma iliyopo Kijiji cha Dule.Wazazi wake wanampenda sana kwa sababu ni mwaminifu.Uaminifu huo umemfanya akubalike katika Kijiji chao na shuleni.Akiwa shuleni,Hawa anasifika kwa kuwa na tabia nzuri ya kutunza mazingira.Pia Hawa ana malengo binafsi yakufanya vyema mtihani wake wa kumaliza muhula wa pili na kuingia darasa la sita.Hawa anapenda masomo ya sayansi na ana ndoto ya kuwa daktari.Mwalimu mkuu alimshauri Hawa ashiriki katika kushauri wanafunzi wenzake wenye tabia ya kukiuka sheria na taratibu za shule.Lengo la ushauri huo lilikuwa ni kubadilisha mienendo yao isiyofaa na kuwa na maadili yanayokubalika shuleni na katika jamii.Hawa alikubali kutekeleza wajibu huo bila kujali jinsi au umri wa wanafunzi husika.

   (i) Kwanini Hawa anakubalika katika Kijiji chao na shuleni?_________________________
   (ii) Kitendo kipi kilimfanya Hawa kusifika shuleni na katika jamii?________________________
   (iii) Mwalimu mkuu alimshauri nini Hawa ili kuboresha na kuimarisha nidhamu ya wanafunzi shuleni?_____________________________________________________________
   (iv) Hawa alitekelezaje wajibu wake wa kubadili menendo isiyo faa kwa wanafunzi wenzake?__________________________________________
   (v) Hawa ana ndoto ya kuwa nani ? ______________________________________________